

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAISI

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA MJI IFAKARA



Tarehe: 14/11/2023

TANGAZO LA KUPATA MAFUNDI WATAKAOFANYA KAZI YA UJENZI WA NYUMBA YA MKURUGENZI NA NYUMBA NNE (4) ZA WAKUU WA IDARA.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imetenga fedha kwa ajili ya Ujenzi wa Nyumba ya Mkurugenzi na nyumba nne za wakuu wa Idara katika Halmashauri ya Mji Ifakara (IFTC). Ujenzi huo utafanywa kwa mfumo wa “**FORCE ACCOUNT.**”

Hivyo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Ifakara, anawatangazia nafasi za kazi kwa mafundi wote wenye uwezo, sifa na uzoefu wa kufanya kazi za ujenzi wa majengo kama vile kujenga, kupaua, kupiga plasta, kufanya (*wiring*), kuweka vigae, kupiga rangi, kuweka milango, madirisha na umaliziaji “finishing” n.k.

SIFA ZA MUOMBAJI (LOCAL FUNDI'S) NA MASHARTI YA KAZI

1. Awe ni raia wa Tanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na awe na kitambulisho cha Taifa au kadi ya Mpiga kura.
2. Awe na uthibitisho wa uzoefu wa kazi za miradi ya ujenzi wa majengo, kwa miradi isiyopungua mitano (5) ya Serikali.
3. Awe na uzoefu wa kujenga nyumba za muundo wa “contemporary”

4. Awe na cheti cha ufundi (fundi ujenzi) "Trade test grade one, two or three" "NVA Level I, II or III", Diploma au Shahada kutoka katika taasisi zinazotambuliwa na Serikali, pia viwe vimethibitishwa na Mwanasheria.
5. Awe tayari kutekeleza kazi ya Ujenzi chini ya msimamizi wa mradi Mhandisi wa Halmashauri ya Mji Ifakara kwa kuzingatia Ramani na BOQ zake.
6. Awe na uwezo wa kusoma na kutafasiri michoro na ramani mbalimbali za Majengo.
7. Awe na kikosi kazi cha mafundi wasiopungua nane (8) na wasaidizi wa fundi wasiopungua watano (5) pamoja na vibarua.
8. Awe na vitendea kazi binafsi vya ufundi kama vile futi kamba, pima maji, kobilo, nyundo, tindo n.k kulingana na kazi atakayofanya.
9. Awe na akaunti hai katika benki ya NMB, NBC au CRDB ambayo inasomeka kwa majina yake na awasilishe Bank statement.
10. Awasilishe gharama za kazi hii kulingana na maelekezo ya kazi husika kwa kujaza fomu ya gharama za mchanganuo wa kazi.
11. Awasilishe mpango kazi na aoneshe mchanganuo wa muda halisi wa kukamilisha kila kazi atakayotakiwa kuifanya.
12. Awe na barua ya utambulisho kutoka Mamlaka ya Serikali za Mitaa, (Kijiji/kitongoji au Mtaa).
13. Awe na TIN namba.
14. Awe na uwezo wa kufanya kazi yeye mwenyewe kama fundi ujenzi.

JINSI YA KUCHUKUA FOMU ZA NUKUU ZA BEI NA KUTUMA MAOMBI


Mwombaji afike ofisi ya Halmashauri ya Mji Ifakara (IFTC) mkabala na Ofisi ya Tanesco Ifakara kuanzia saa **2:00 asubuhi** hadi saa **9:00 alasiri** siku za kazi, ili kuchukua fomu za nukuu za bei ya ufundi (Quotation Form), katika ofisi ya Manunuzi, na afike kuanzia saa **200:00 asubuhi** hadi saa **9:00** ili kupata ufafanuzi wa kazi, maelezo ya ziada na kuona eneo la kujenga katika ofisi ya Ujenzi. Fomu za nukuu za bei zitapatikana bila malipo. Muombaji akishajaza nukuu za bei ya ufundi (Quotation Form) aambatanishe na barua ya kuomba kazi na kisha azifunge vizuri kwenye bahasha. Juu ya bahasha aandike **Maombi ya Ujenzi wa Nyumba ya mkurugenzi na Nyumba nne (4)** za wakuu wa Idara Halmashauri ya Mji Ifakara. Kila ombi liwekwe katika bahasha yake zikiwa na **nakala mbili**.

Barua zote za maombi ya kazi ziwasilishwe Ofisi ya Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Ifakara kupitia anuani ifuatayo:

Mkurugenzi wa Mji,
Halmashauri ya Mji Ifakara,
S.L.P 433,
Ifakara.

Maombi ya kazi ya ujenzi yataanza kupokelewa tarehe 15/11 /2023 kuanzia saa 02:30 asubuhi hadi saa 09:30 jioni, mwisho wa maombi tarehe 21/11/2023 saa 6:30 mchana.

Tangazo limetolewa na:


Rashid Semngoya
KAIMU MKURUGENZI WA MJI
IFAKARA

